



# MIFUMO YETU

Jarida la Mifumo ya TEHAMA ya TAMISEMI




TOLEO NA. 1

MEI-JULAI, 2017



**Uzinduzi wa Tovuti kwenye  
Mikoa na Halmashauri zote  
Nchini**



*Picha ya mbele: Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais—Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. George Simbachawene, akibonyeza kompyuta kuashiria uzinduzi wa tovuti za Mikoa na Halmashauri, katika hafla iliyofanyika mjini Dodoma Machi 27, 2017. Wengine kutoka kushoto ni: Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mhe. Said Meck Sadiki, Afisa Habari kutoka Wakala ya Serikali Mtandao (eGA), Rainer Budodi, Kaimu Afisa Habari wa Halmahsauri ya Wilaya ya Singida, Victor Alexander, na Mkurugenzi Msaidizi wa USAID/Tanzania, Timothy Donnay. (Picha kwa hisani ya Mroki Mroki wa Habari Leo).*

*Jarida hili limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI, na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).*

*“Jarida hili limefanikishwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), kupitia Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3). Ofisi ya Rais -TAMISEMI ndiyo itakayowajibika na matokeo ya kazi hii. Jarida hili ni maoni ya mtayarishaji, na si lazima liwakilishe maoni ya USAID au Serikali ya Marekani”*



**USAID/TANZANIA UIMARISHAJI WA MIFUMO YA  
SEKTA ZA UMMA**



# Bodi ya Uhariri

## Mwenyekiti

*Eng. Mussa Iyombe*  
*Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, TAMISEMI*

## Wajumbe

*Erick Kitali – TAMISEMI*  
*Mtani Yangwe – TAMISEMI*  
*Baltazar Kibola – TAMISEMI*  
*Rebecca Kwandu – TAMISEMI*  
*Desderi Wengaa – PS3*  
*Revocatus Mtesigwa – PS3*

## Waandishi

*Mathew Kwembe – TAMISEMI*  
*Gladys Mkuchu – PS3*  
*Jacqueline Sombe – PS3*

## Mhariri Mkuu

*Leah Mwainyekule – PS3*

## Wahariri

*Erick Kitali – TAMISEMI*  
*Mathew Kwembe – TAMISEMI*  
*Dr. Conrad Mbuya – PS3*

## Msanifu Kurasa

*Leah Mwainyekule*

## Jarida hili hutolewa na:

*Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – TAMISEMI*  
*S.L.P 1923*  
*Dodoma – Tanzania*  
*Simu: (+255) 26 – 2321234*  
*Barua pepe: ps@tamiseemi.go.tz*  
*Tovuti: www.tamiseemi.go.tz*

## Ndani ya Jarida Hili:

Tovuti zitoe taarifa kwa wakati	uk 7
Serikali yaishukuru USAID kuisogeza kwa wananchi	uk 8
Mfumo wa tovuti mpya kurahisisha kazi za wataalam	uk 9
Agizo kwa tovuti mpya kuwa na taarifa mpya	uk 10
PS3 yafanikisha uundwaji tovuti mpya za Serikali	uk 11
Wananchi wafurahia upatikanaji wa taarifa	uk 12
eGA yawahakikishia wadau huduma za uhakika	uk 13
Maafisa Habari na TEHAMA watoa pongezi	uk 15
DC Kigoma aagiza Maafisa Habari wapewe ushirikiano	uk 16
Maafisa watakiwa kutumia njia za kisasa za mawasiliano	uk 17
Mahojiano maalum na Waziri Simbachawene	uk 18
Matukio mbalimbali wakati wa uzinduzi wa Kitaifa	uk 22

**TAHARIRI:**

## Tovuti mpya za Serikali ziwe chachu ya maendeleo

Mpendwa Msomaji, karibu katika toleo hili la kwanza la Jarida la *Mifumo Yetu* ambalo linatayarishwa kwa pamoja kati ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, na Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3).

Katika toleo hili la kwanza, Jarida linalenga kuhabarisha umma kuhusu maendeleo na matokeo yaliyotokana na utekelezaji wa utayarishaji wa mfumo mpya wa tovuti za Serikali, unaojulikana kwa Kiingereza kama “*Government Website Framework (GWF)*.” Mfumo huu umeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Wakala ya Serikali Mtandao (eGA), OR-TAMISEMI na PS3, na tayari Mikoa 26 na Halmashauri zake zote 185 kutoka Tanzania bara, zimekwishandaa tovuti zake.

Uandaaji wa tovuti hizi umefadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kupitia Mradi wa PS3, na unalenga kuboresha huduma katika sekta za umma kwa kumwezesha mwananchi kupata taarifa sahihi na kwa haraka. Aidha, unalenga pia kuiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake katika njia ya uwazi, hivyo kuboresha utawala bora na utoaji wa huduma mbalimbali za sekta za umma na kuifanya Serikali iwajibike zaidi kwa wananchi inaowatumikia.

Ingawa Mradi wa PS3 unafanya kazi ndani ya Halmashauri 93 katika Mikoa 13 ya Tanzania bara, kutokana na uandaaji wa tovuti kuwa muhimu kwa kila raia wa Tanzania, tunayo furaha kukueleza kwamba Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), imetuwezesha kufanikisha mafunzo na uandaaji wa tovuti katika Halmashauri 185 na Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, bila kubagua. Mikoa na Halmashauri ambazo hazipo chini ya Mradi ziliweza kuwaghamia wataalam wake kuhudhuria mafunzo ya uandaaji wa tovuti, pamoja na kuhakikisha kwamba malipo yanafanyika kwa ajili ya tovuti hizo kuwa hewani.

Kupitia Jarida hili ambalo litakuwa likitolewa kila baada ya miezi mitatu, mpendwa msomaji utapata fursa ya kujua maendeleo na hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa kuimarisha mifumo mbalimbali ya Serikali. Utafahamishwa pia mafanikio na changamoto mbalimbali zitakazokua zinajitokeza, katika utekelezaji wa mradi huu.

Ni imani yetu kwamba Jarida hili litakupa fursa kubwa ya kufahamu namna Serikali inavyowafikia wananchi wake kwa haraka kupitia mfumo huu wa tovuti katika kila Mkoa na kila Halmashauri, ili kusaidia kupeleka taarifa kwa upana na haraka zaidi kwa wananchi.

Rai yetu kwa Maafisa Habari wa Mikoa na Halmashauri ni kwamba wahakikishe kuwa tovuti za Mikoa na Halmashauri zimesheheni taarifa mpya, zilizotolewa kwa wakati. Vilevile, tunawasihi Maafisa wa Serikali katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuondoa urasimu katika kutoa taarifa, ili tovuti hizi zitumike kweli kwa malengo yaliyokusudiwa.

Tunawatakiwa usomaji mwema!



**Eng. Mussa Iyombe**  
Katibu Mkuu, OR-TAMISEMI

## KUTOKA DODOMA:

## ‘Tovuti za Mikoa na Halmashauri zitoe taarifa kwa wakati’


**W**aziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) Mhe. George Simbachawene, amezitaka Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwawezesha Maafisa Habari waliopo chini ya ofisi zao kutekeleza majukumu yao kwa wakati na haraka ili kuendana na kasi ya ukuaji wa kiteknolojia na kupashana habari ili kuwaletea Wananchi maendeleo.

Mheshimiwa Simbachawene ameyasema hayo mjini Dodoma wakati akizindua tovuti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo zitatumika katika uwasilishaji wa habari na taarifa muhimu kwa Wananchi.

"Nawaagiza Wakuu wa Mikoa wote kuhakikisha wanawanunulia Maafisa Habari katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa vifaa hivi muhimu kama kamera, kompyuta, mtandao wa intaneti na vingine vya kufanyia kazi hizi muhimu ndani ya miezi mitatu kuanzia sasa, na kwa gharama ya ofisi zao, ili waweze kuwapatia wananchi taarifa ikiwa ni haki yao ya msingi ya kupata taarifa," alisema Mhe. Simbachawene.

Mhe. Simbachawene amesema kwakuwa Tanzania iliweka sainsi Azimio la 'Open Government Partnership' mwaka 2011, kuweka uwazi wa shughuli za Serikali kwa wananchi, ikiwa na lengo la kuimarisha utawala bora, kuondoa rushwa na kujenga imani kwa wananchi wake, Azimio linaweka msisitizo kwa wananchi kupata taarifa kwa wakati na uhuru zaidi.

Aidha Mhe. Simbachawene amewataka Maafisa Habari wa Mikoa na Halmashauri kuhakikisha kwamba tovuti zao zinakuwa



**Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI, Mhe. George Simbachawene (wa tatu kutoka kushoto) akiangalia tovuti ya Manispaa ya Dodoma wakati wa hafla ya uzinduzi iliyofanyika Machi 27, 2017, mjini Dodoma. Wengine kutoka kushoto ni: Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mhe. Said Meck Sadiki, Waziri wa Habari, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe, Kaimu Afisa Habari wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Victor Alexander, na Mkurugenzi Msaidizi wa USAID/Tanzania, Timothy Donnay. (Picha kwa hisani ya Mroki Mroki, Habari Leo)**

na taarifa sahihi na za kutosha, na ziwe zinatolewa kwa wakati.

Pia amewataka watendaji katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuondoa urasimu katika kutoa taarifa.

"Lazima taarifa zitolewe kwa wakati ili tovuti hizi zitumike kweli kwa malengo yaliyokusudiwa," alisisitiza Mheshimiwa Simbachawene.

Waziri Simbachawene aliwashukuru Watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kwa kuwezesha mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) ambao kupitia ufadhili huo umeweza kuendesha mafunzo ya utengenezaji wa tovuti hizo.

Kwa upande wake, Waziri wa Habari,

Sanaa, Utamaduni na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe, amewaelekeza Maafisa Habari kutowaangusha wananchi na kuhakikisha wanawapa taarifa pasipo urasimu wowote.

Waziri Mwakyembe amewasisitiza Maafisa Habari kuhakikisha kuwa tovuti hizo hazigeuki kuwa magofu ya habari, bali majokofu ya habari kwa kupata habari mpya kila siku.

Katika mafunzo hayo, Maafisa Habari, na Maafisa TEHAMA kutoka Halmashauri 185 na Mikoa 26 walishiriki mafunzo hayo na kufundishwa namna ya kuandaa taarifa mbalimbali katika tovuti zao.

**Chanzo: Hotuba ya Uzinduzi wa Tovuti**

## Serikali yaishukuru USAID kwa kuisogeza karibu na wananchi

**S**erikali imelishukuru Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kupitia Mradi wake wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), kwa kufadhili Mafunzo kwa Maafisa Habari na TEHAMA, pamoja na kufanikisha uundaji wa tovuti za Mikoa na Halmashauri.

Mkurugenzi wa Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Erick Kitali, ameyasema hayo wakati wa mahojiano maalum na mwandishi wa jarida hili, juu ya tovuti mpya za Mikoa na Halmashauri.

Amesema kuwa Mradi wa PS3 umeiwezesha Mikoa na Halmashauri kuwa na tovuti zake, na pia kutoa gharama za mafunzo kwa Maafisa Habari na TEHAMA, jambo ambalo lingeiharimu Serikali fedha nyingi.

“Bila msaada wa PS3 tusingekuwa hapa

tulipo, hivyo basi ni wajibu wa kila Mkoa na Halmashauri kuhakikisha kuwa tovuti hizi zinaendelea kuwa hewani na taarifa muhimu na zinazoendana na wakati zinawekwa,” alisema.

Bwana Kitali ameongeza kuwa tayari PS3 imefanya kazi kubwa ya kutoa mafunzo na kulipia matumizi ya tovuti hizo, na kwamba Mradi huo pia utalipa gharama za uendeshaji wa tovuti za Halmashauri zilizo ndani ya mikoa 13 ya PS3 kwa muda wa mwaka mmoja, na baadaye Mikoa na Halmashauri hizo kuendelea kulipa gharama hizo kupitia vyanzo vyao vya mapato.

Mkurugenzi huyo wa TEHAMA amesema kuwa kwa muda mrefu Serikali ilikusudia kuwa na tovuti kwa kila Mkoa na Halmashauri nchini kote, lakini mkakati huo ulisuasua kutokana na kutoku-

wa na fedha za kutosha kwa wakati huo kulitekeleza.

Bwana Kitali ameongeza kuwa zipo faida nyingi zitokanazo na kuwa na tovuti katika Halmashauri nchini, mathalani tovuti hizo kutumika kama chombo bora cha utoaji taarifa kwa wananchi.

“Wananchi hawatahitaji tena kupanga foleni na kupoteza muda wao mwingi katika ofisi mbalimbali za Halmashauri wakihitaji taarifa ama wakihitaji fomu za maombi mbalimbali kama umiliki wa ardhi na leseni za biashara ndani ya maeneo yao, kwani taarifa hizo zote zitapatikana katika tovuti,” alisisitiza bwana Kitali.

Amesema kuwa Serikali imelenga kuona kuwa kila Mkoa na Halmashauri nchini inakua na tovuti yake ili kuiwezesha kuwasiliana na watu wake kwa urahisi na kwa uwazi, ikiwa ni sehemu muhimu katika utekelezaji wa dhana ya utawala bora.

“Halmashauri ni ngazi muhimu sana katika Serikali, kwani huko ndiko wananchi walipo, hivyo kuna uhitaji mkubwa wa kuwarahisishia wananchi kuifikia Serikali yao na Serikali kufikia watu wake kupitia tovuti,” alisema bwana Kitali.

Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), lilifanikisha uundwaji wa tovuti hizo kupitia mfumo wa utengenezaji wa tovuti za Serikali, yaani ‘Government Website Framework’ (GWF), ambapo Maafisa Habari na TEHAMA kutoka Mikoa 26 na Halmashauri 185 walipatiwa mafunzo.

*Imeandikwa na Jacqueline Sombe, PS3*



**Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) katika Ofisi ya Rais—TAMISEMI, Erick Kitali, akifanyiwa mahojiano hivi karibuni jijini Mwanza. (Picha na Leah Mwainyekule, PS3)**



## Mfumo wa tovuti za Serikali kurahisisha kazi za wataalam

**M**fumo wa Tovuti za Serikali (GWF) ambao upo chini ya Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) umelenga kuiwezesha Mikoa na Halmashauri kuwa na tovuti zenye muonekano wa kufanana ili kurahisisha utatuzi wa pamoja pindi matatizo ya kitaalam yanapojitokeza.

Kwa mujibu wa mmoja wa wakufunzi wa mafunzo ya uundaji wa tovuti hizo, Bwana Rainer Budodi, mbali na kurahisisha utatuzi wa changamoto, mfumo wa tovuti hizo mpya licha ya kufanana, muonekano wake umerahisishwa ili kumpa mtumiaji urahisi wa kupata taarifa.

Bwana Budodi ambaye pia ni Afisa Habari wa eGA ameipongeza hatua ya Serikali kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) kuandaa tovuti hizi. Amesema hii ni ishara kwa serikali kujipanga upya na kuboresha mifumo yake ya mawasiliano kwa wananchi kwa kufuata ulimwengu wa digitali.

“Tovuti hizi zitapunguza kwa kiasi kikubwa mianya ya rushwa, ambapo baadhi ya watu wasiokuwa waaminifu walijenga tabia ya kuwatoza wananchi vitu kama fomu ambazo kihalali ilibidi kutolewa bure kwa wananchi. Vilevile, tovuti hizi zitapunguza urasimu usio na msingi pamoja na ucheleweshwaji wa huduma,” ameingiza Budodi.

Ameeleza kwamba tovuti hizi pia zitapunguza “kazi za makaratasi” (*paperwork*) na usumbufu wote wa watu kupanga foleni kwa ajili ya mauzo kwa taarifa zote, kwani tayari tovuti zitakuwa ni jukwaa la kujibu maswali, kupokea malalamiko na kutoa taarifa.

Bwana Budodi pia amepongeza jitihada za kuwaleta na kuwaweka pamoja Maafisa Ha-



**Afisa Habari kutoka Wakala ya Serikali Mtandao (eGA), Rainer Budodi, akitoa mada wakati wa mafunzo wa uundaji wa tovuti jijini Mwanza. (Picha na Jacqueline Sombe, PS3)**

bari na Maafisa TEHAMA, kwakuwa taaluma hizi zina uhusiano wa karibu sana kati ka kuwafikishia wananchi taarifa, hivyo zinapofanya kazi kwa ushirikiano na kutumia ujuzi wao kwa pamoja matokeo yake huwa chanya.

Kwa upande wake, Afisa TEHAMA kutoka eGA, Mhandisi Donald Samwel, amesema changamoto kubwa iliyokuwepo katika Halmashauri nyingi ni kukosekana kwa taarifa za kuweka katika tovuti, hasa kwa Halmashauri ambazo hazikuwa na tovuti kabisa. Halmashauri zilizokuwa nazo, tovuti hizo hazikuwa rahisi kutumiwa.

Akieleza kuhusu tofauti iliyopo kati ya tovuti mpya za Serikali na zile za zamani, Mhandisi Samwel amesema kuwa tovuti za zamani kwa Halmashauri zilikuwa ni tovuti zisizobadilika na hazikuwa na nafasi

ya kufanya mabadiliko, tofauti na hizi mpya ambazo zina nafasi ya kubadilisha taarifa pasipo kufuata mlolongo mrefu.

“Katika tovuti hizi mpya za Serikali, mtu yeyote ambaye amepewa mamlaka ya kuwa msimamizi ana uwezo wa kuitanua tovuti yake kwa kuongeza kurasa, viunganishi, kuweka na kuhuisha taarifa kwa kadri atakavyoweza,” amesema.

Amesema kuwa tovuti hizi zimetoa nafasi ya kushirikishana taarifa, hivyo kuifanya Halmashauri husika kutambulika na kukua. Vilevile, inakuwa ni jukwaa la kutangaza fursa mbalimbali zilizopo katika Halmashauri na kukuza shughuli za kiuchumi zilizopo.

***Inaendelea ukurasa wa 10***

**KUTOKA MOROGORO:**

## Agizo kwa tovuti kuwa na taarifa mpya kila wiki

**M**aafisa TEHAMA na Mawasiliano wameagizwa kuhakikisha kila mwisho wa wiki Tovuti zao zinakuwa na taarifa mpya. Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Dkt. John Ndunguru, ametoa agizo hilo wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa Maofisa Habari na TEHAMA wa Halmashauri na Mikoa ya Morogoro, Kilimanjaro, Arusha na Tanga, Machi 20, 2017 mkoani Morogoro.

“Inapofika ijumaa (Machi 27), tovuti ya kila Halmashari na Mkoa inabidi iwe na taarifa mpya naielezee shughuli zote zilizotendeka na taarifa nyingine yoyote ambayo wananchi wana haki ya kupata,” alisema Mhandisi Dkt. Ndunguru.

Vilevile, Dkt. Ndunguru ameeleza kwamba moja ya haki ya Kikatiba waliyonayo

wananchi ni haki ya kupata taarifa, hivyo kwa kutokutoa taarifa zilizo sahihi na kwa wakati, wananchi wanakuwa wamenyimwa na kukoseshwa haki yao ya kikatiba. Kutokana na hilo, ameagiza kila afisa aliye hudhuria mafunzo hayo ahakikishe anawapa wananchi wake haki yao ya kikatiba ya kupata taarifa.

Aidha, Katibu Tawala huyo amesisitiza kuwepo na ushirikiano baina ya Maofisa TEHAMA na Habari katika utendaji kazi wao wa kila siku, na kufikia malengo yao, ili kuweza kwenda sambamba na sera ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Hapa Kazi Tu.

Awali, Meneja Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) mkoa wa Morogoro, Bw. David Ole Laput, alisema kuwa PS3 ni mradi unaofadhiliwa

na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), na unafanya kazi na Serikali Kuu pamoja na Halmashauri 93 katika mikoa 13 ya Tanzania bara ili kuboresha mifumo ya umma. Pia kupitia mradi, huo maofisa hao watajengewa uwezo wa kutengeneza tovuti, kuweka taarifa sahihi kwenye tovuti, na kutangaza huduma mbalimbali wanazotoa kupitia tovuti hizo.

Mafunzo hayo ya wiki moja ya kikanda yaliyoenda sambamba katika mikoa ya Dodoma, Mtwara, Kigoma na Morogoro, yalifikia kilele chake Machi 27, 2017 kwa uzinduzi rasmi wa Tovuti za Halmashauri na Mikoa yote Tanzania bara.

**Chanzo: tovuti ya eGA**

## Mfumo wa tovuti mpya kurahisisha kazi za wataalam

### **Inatoka ukurasa wa 9**

Kwa upande wake, Afisa TEHAMA wa mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Albert Macha, ameeleza kuwa zamani usimamizi wa tovuti katika mkoa wake ulikuwa chini ya mtu binafsi, jambo lililokua likisababisha tovuti ya mkoa wa Shinyanga kutokuwa hewani kwasababu ya kuvamiwa mara kwa mara na wahalifu wa mitandao, hivyo kupunguza ufanisi na utegemezi katika tovuti ya mkoa wake.

“Lakini ninaamini sasa tovuti ya Mkoa wa

Shinyanga itakuwa salama, kwani usimamizi utakuwa chini ya chombo cha Serikali kinachoaminika,” ameeleza.

Naye Afisa Habari wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Stephen Msengi, ameeleza matumaini yake kuwa tovuti hizi mpya zitarahisisha huduma zitolewazo na Serikali kwa wananchi, kwani baadhi ya huduma hizi sasa zitapatikana kupitia tovuti.

“Kero kwa wananchi kuhusu kupata taarifa zitapungua kwa kiasi kikubwa au

kuisha kabisa, kwani watapata taarifa zote kupitia tovuti, na kwa mtazamo wangu, ninaona hii ni hatua kubwa sana kwa Serikali,” ameeleza.

Kulingana na takwimu za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), jumla ya wataalam milioni 19 hutumia huduma za mtandao ili kujipatia habari ikiwemo kupitia tovuti mbalimbali na blogu, kusoma barua pepe, kutembelea kurasa za kijamii kama Facebook.

**Imeandikwa na Jacqueline Sombe, PS3**

## PS3 yafanikisha uundwaji wa tovuti za Serikali

**M**radi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) umefanikisha uandaaji wa tovuti zote za Mikoa 26 na Halmashauri zake 185 za Tanzania bara.

Mradi huu ambao unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID), umefanikisha uandaaji wa tovuti hizo kupitia Mwongozo wa uandaaji wa tovuti za Serikali yaani 'Government Web-site Framework' (GWF).

Kiongozi wa Timu ya Mifumo ya Mawasiliano wa PS3, Desderi Wengaa, amesema kuwa mradi wa PS3 unalenga kuboresha huduma katika sekta za umma kwa kumuwezesha mwananchi kupata taarifa sahihi, kwa haraka na kwa wakati.

"Kitengo cha Mifumo ya Mawasiliano, na Kitengo cha Utawala Bora na Ushirikishwaji wa Wananchi vya PS3, viliona ni vema kuzifanyia kazi changamoto za mifumo ya TEHAMA katika taasisi za Serikali ambazo zinazuia upatikanaji wa haraka wa taarifa kwa wananchi," ameeleza.

Amesema lengo la PS3 ni kuona kuwa Serikali inawafikia wananchi kwa haraka kupitia mfumo huo ambao utasaidia kupeleka taarifa kwa ukamilifu na haraka zaidi.

Bwana Wengaa ameongeza kuwa utafiti walioufanya umetoa hamasa kwa Serikali ya Marekani kupitia Shirika lao la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), kuona haja ya kusaidia kuboresha mifumo hiyo, ambapo mojawapo ya mipango hiyo ni kuwezesha uandaaji wa tovuti za Mikoa na Halmashauri.



**Kiongozi wa Timu ya Mifumo ya Mawasiliano wa PS3, Desderi Wengaa, akiwasilisha mada katika moja ya mikutano ya PS3. (Picha kutoka maktaba ya PS3)**

Ameongeza kuwa lengo ni kuiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake katika njia ya uwazi ambalo moja ya matakwa ya utawala bora, hivyo kuboresha huduma mbalimbali za sekta za umma na kuifanya iwajibike kwa wananchi inaowatumikia.

Naye Meneja wa Mifumo ya Mawasiliano wa PS3, Revocatus Mtesigwa, amesema kuwa moja ya mambo ambayo waliyabaini wakati wa utafiti wa kutathmini upungufu uliopo katika mifumo ya TEHAMA ndani ya taasisi za Serikali, hususan katika tovuti, ni kuto-kuwa na umiliki wa moja kwa moja wa tovuti hizo.

Amesema kuwa PS3 kwa kushirikiana na TAMISEMI pamoja Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) waliona ni vye-

ma watumie rasilimali watu walioko ndani ya Mikoa na Halmashauri husika kwa ajili ya kuandaa mfumo huo, ambao wataweza kutatua changamoto zitakazojitokeza wakati wa kuandaa tovuti hizo, kuzisimamia na kuziendeleza.

Kuanzishwa kwa mfumo huu mpya kutarahisisha utunzaji, kwani tovuti zilizoundwa kupitia mfumo huu zitahifadhiwa katika mitambo ya ofisi za eGA na hivyo kuzifanya tovuti kuwa endelevu, tofauti na awali ambapo taasisi hizo zilitumia taasisi binafsi kuendesha tovuti hizo na hivyo kutumia rasilimali fedha nyingi na hata kushindwa kuziendesha.

**Imeandikwa na Gladys Mkuchu, PS3**

**KUTOKA MTWARA:**

## Wananchi wafurahia upatikanaji wa taarifa kupitia tovuti za Mikoa na Halmashauri

**W**ananchi mkoani Mtwara wamepongeza mchakato wa uandaaji wa tovuti za Mikoa na Halmashauri, wakisema utarahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa haraka kutoka katika Mamlaka hizo za Serikali za Mitaa.

Aidha, wamesema kuwa hatua hiyo itachochea shauku ya wananchi kufahamu mambo mbalimbali yanayohusu maeneo yao, pamoja na kupata majibu ya maswali na changamoto mbalimbali zinazowakabili kupitia Serikali Kuu.

Wakitoa maoni yao mara baada ya tovuti hizo kuwa hewani rasmi kufuatia kukamilika kwa mafunzo ya Maafisa Habari na TEHAMA yaliyoenda sambamba na uandaaji wa tovuti za Mikoa 26 na Halmashauri zote 185 nchini hivi karibuni, wananchi hao wamesema kuwa taarifa hizi zitachochea uwazi, uwajibikaji wa viongozi na utawala bora.

Mmoja wa wananchi hao, Bwana Chande Athumani, ameelezea kufurahishwa kwake na taarifa za kuwepo kwa tovuti hizo, na kudai kuwa hapo awali ilikuwa ni vigumu kupata taarifa muhimu ambazo wananchi walizihitaji. Ameongeza kwamba ilikuwa inachukua muda mrefu sana kwa mamlaka mbalimbali husika kutoa taarifa hizi kwa wananchi, na wakati mwingine ililazimu wananchi kuzifuata kwenye ofisi husika.

“Tunaamini kupitia tovuti hizi upatikanaji wa taarifa mbalimbali kama vile namna ya kuweza kupata taarifa ya kulipia leseni na kukata bima kupitia viunganishi vya haraka na kupata maelekezo na huduma mbalimbali tunazozihitaji wananchi kutoka katika Halmashauri zetu, utakuwa umerahisishwa sana. Tunatumai wananchi hatutalazimika

kufuata fomu hizo ofisini, isipokuwa tutakuwa tunazitoa kwenye mtandao,” amesema.

Bwana Chande ambaye pia ni Mwenyekiti wa waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda mkoani Mtwara, ameongeza kuwa huduma hiyo itaokoa muda wao wa kupanga foleni ndefu kwenye Mamlaka husika ili kupata huduma hizo.

Mkazi mwingine, Bi Neema Barnaba, amesema kuwepo kwa tovuti katika halmashauri yake kutamuwezesha yeye binafsi kupata taarifa sahihi kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri yake, na hivyo kumuondolea kero ya upotoshaji au ucheleweshaji wa huduma pindi anapolazimika kuulizia kwa watu.

Amesema kuwa kabla ya kuwepo kwa

tovuti katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, alikuwa akilazimika kwenda katika ofisi za kijiji ili kuweza kupata taarifa alizokuwa aki-zihitaji, lakini anashukuru kuwa sasa taarifa hizo atakuwa akizipata moja kwa moja katika tovuti ya Halmashauri yake.

Ameongeza kuwa huduma ya tovuti ni muhimu kwao kwani pia itaondoa suala la ucheleweshaji wa kufanyia kazi baadhi ya taarifa wanazozihitaji, ambazo mara nyingine huwa haziwekwi katika mbaao za matangazo ya ofisi za Vijiji, Halmashauri na Mikoa.

“Muda mwingi wananchi tumekuwa na uhitaji wa kufahamu mambo mbalimbali kwenye Halmashauri zetu na mikoa, lakini tunashindwa kufahamu mahali sahihi pa kupata taarifa hizi.

*Inaendelea ukurasa wa 14*



**Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mhe. Halima Dendegu, akizungumza katika tukio la uzinduzi wa Mradi wa PS3 mkoani Mtwara, mwaka 2016. (Picha kutoka maktaba ya PS3)**

## Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) yawahakikishia wadau wake huduma za uhakika



**Mtendaji Mkuu wa eGA, Dkt. Jabir Bakari, akisoma hotuba fupi wakati wa hafla ya uzinduzi wa tovuti za Mikoa na Halmashauri mjini Dodoma, Machi 27, 2017. (Picha kwa hisani ya Mroki Mroki, Habari Leo)**

**W**akala ya Serikali Mtandao (eGA) imewahakikishia wadau wake kuwa imejiandaa vema kusimamia na kuhifadhi tovuti zote za Serikali ili ziweze kufanya kazi kwa uhakika kwa saa 24 kwa siku 7, tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

Mtendaji Mkuu wa eGA, Dkt. Jabir Bakari, ameyasema hayo mjini Dodoma wakati wa uzinduzi rasmi wa tovuti za Mikoa na Halmashauri, uliofanyika Machi 27, 2017.

Amesema kuwa eGA imejiandaa vema katika kusimamia na kuhifadhi tovuti zote 211 katika vituo maalum vya kuhifadhia na kuendesha mifumo mbalimbali ya Serikali Mtandao.

Dkt Bakari ameongeza kuwa utaratibu huu wa kuhifadhi tovuti ni tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo kila taasisi ilihifadhi

tovuti yake yenyewe, na hivyo kusababisha tovuti nyingi kutokuwa hewani pindi zinapopata hitilafu yoyote kwenye miundombinu kama vile kukatika kwa umeme.

Mbali na changamoto hiyo, Dkt Bakari ameeleza kwamba Mikoa na Halmashauri nyingi hazikuwa na tovuti zake. “Hapo awali Mikoa na Halmashauri nyingi zilikuwa hazina tovuti, na zile zilizokuwa nazo, hazikufanya kazi vizuri, na wakati mwingine hazikupatikana kabisa. Hata taarifa zake zilikuwa hazindani na wakati, na nyingine zilikuwa na anwani zenye kikoa cha *dot.com* badala ya kuonyesha umiliki wa taasisi ya umma,” amesema.

Ameongeza kuwa moja ya hatua za utekelezaji wa Serikali Mtandao ni ku-

wa na uwezo wa kupata taarifa na huduma mbalimbali kwa njia ya mtandao kwa urahisi, haraka, gharama nafuu wakati wowote na mahali popote.

“Ili kukamilisha azma hiyo, Wakala ya Serikali Mtandao ikishirikiana na TAMISEMI, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa Michezo na Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), tovuti za mikoa yote 26 na Halmashauri 185 za Tanzania bara zimeandaliwa,” alisema.

Dkt. Bakari amesema kuwa Maafisa TE-HAMA na Maafisa Mawasiliano 422 kutoka katika Mikoa na Halmashauri hizo wamepata mafunzo ya kutengeneza muonekano wa tovuti zao na kuweka taarifa kwa ajili ya umma wakiwa mahali popote na wakati wowote kwa kutumia mfumo mpya wa tovuti.

“Tovuti hizi pia zitaunganishwa na Tovuti Kuu ya Serikali [www.tanzania.go.tz](http://www.tanzania.go.tz) ambayo ndiyo dirisha moja la kutolea taarifa na huduma za Serikali kwa umma.” amesisitiza.


Pia Dkt Bakari ameushukuru Mradi wa PS3 na viongozi wake kwa kufadhili shughuli ya kuimarisha mifumo inayoboresha utendaji kazi na inayorahisisha upatikanaji wa taarifa na huduma kwa umma.

Wakala ya Serikali Mtandao inaaahidi kuen-delea kutoa ushauri na msaada wa kiufundi kwa Mikoa na Halmashauri zote nchini zinazotumia Mfumo wa Tovuti za Serikali (GWF) ili kuhakikisha mfumo unafanya kazi kwa ufanisi zaidi.

***Imeandikwa na Mathew Kwembe,  
TAMISEMI***

## Wananchi wafurahia upatikanaji wa taarifa

*Inatoka ukurasa wa 12*



**Baadhi ya wakurufunzi wa tovuti za Mikoa na Halmashauri, wakiandaa tovuti zao wakati wa mafunzo yaliyofanyika jijini Mwanza, mwezi Februari, 2017. (Picha na Leah Mwainyekule, PS3)**



**Wakurufunzi kutoka PS3, Giovanni DiPiazza (kushoto) na Fenohasina Rakotondrazaka Maret, katika moja ya madarasa ya mafunzo ya tovuti, jijini Mwanza. (Picha na Jacqueline Sombe, PS3)**

na mara nyingi hata ukhitaji kuonana na viongozi inakuwa ngumu sana kupatiwa nafasi ya kuonana nao ili kufahamu mambo mbalimbali. Lakini tunaamini mchakato huu wa kuwepo na tovuti hizi utatuwezesha kufahamu mambo mbalimbali muhimu na hata kutoa maoni yetu ili yaweze kufanyiwa kazi na ngazi husika Serikalini,” amesema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mhe. Halima Dendegu, ameushukuru Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) pamoja na Wizara shirikishi kwa kuja na wazo la kuandaa tovuti za Mikoa na Halmashauri.

“Tovuti hizi zitatoa fursa kwa wananchi kujifunza na kupata taarifa mbalimbali kuhusu Mkoa na Halmashauri zao. Ni fursa pia kwa watu wengine kujua taarifa mbalimbali kuhusu Mtwara. Hii itasaidia pia kutangaza fursa za uwekezaji katika tovuti zetu kulingana na rasilimali zilizoko katika

mkoa wetu, ili kutekeleza kaulimbiu ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na Serikali ya viwanda, na hivyo kusaidia kuwepo kwa huduma mbalimbali karibu na wananchi,” ameingiza Mh. Dendegu.

Mh. Dendegu pia amewaasa Maafisa Habari na Tehama kutambua mipaka yao ya kazi, lakini kutokuwa na uoga wa kufuatilia na kutoa taarifa mbalimbali zenye faida kwa manufaa ya wananchi, na kutoogopa kuwafuata viongozi kwa ajili ya kupata taarifa na kuwaomba viongozi kuweza kutoa ushirikiano pamoja na kuwapatia taarifa stahiki ili kuchochea uwazi na uwajibikaji.

Naye Mshauri wa Masuala ya Utawala Bora na Ushirikishwaji wa wananchi kutoka Mradi wa PS3 mkoani Mtwara, Bwana Eusebi Kapilima, amesema kuwa uwepo wa tovuti katika Mikoa na Halmashauri ni upigaji wa hatua kikatiba,

kwani imewapa wananchi fursa ya kupata taarifa zinazowahusu.

Amesema, kwakuwa Serikali inawajibika kuwa wazi kwa wananchi wake kutoka ngazi za chini za Serikali za Mitaa hadi Serikali Kuu kama vile taarifa za umiliki wa ardhi, kufahamu kiasi cha bajeti kilichopangwa kwa ajili ya Halmashauri zao na huduma mbalimbali, hivyo ni fursa ya wao kuhoji pale ambapo mambo hayaendi sawa.

Uandaaji wa tovuti za Mikoa 26 na Halmashauri 185 pamoja na Mafunzo kwa Maafisa Habari na TEHAMA wa Mikoa na Halmashauri, ulifadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), ikishirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao (eGA) na Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

**Chanzo: Channel Ten**

## KUTOKA MBEYA:

## Maafisa Habari na TEHAMA wapongeza juhudi za PS3 kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wananchi

**M**aafisa Habari na TEHAMA kutoka Halmashauri za Mikoa ya Mbeya, Njombe, Rukwa na Songwe, wamepongeza jitihada zilizofanywa na Serikali kwa kushirikiana na Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) ya kuwapa mafunzo ya kuandaa tovuti.

Maafisa hao wametoa pongezi hizo hivi karibuni mara baada ya kushiriki mafunzo ya kuandaa tovuti ambayo yalienda sambamba na kuandaa tovuti za Mikoa na Halmashauri yaliyofanyika katika jiji la Mbeya.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Afisa TEHAMA kutoka Mkoa wa Njombe, Mhandisi Peter Mkumbo, amesema mafunzo hayo yatasaidia uboreshaji wa utoaji wa huduma kwa jamii na kuongeza uwajibikaji wa watumishi katika ofisi za Serikali.

“Naipongeza Serikali kupitia TAMISEMI na Wakala ya Serikali Mtandao eGA kwa kushirikiana na mradhi wa PS3 kwa kuja na huu mfumo wa Government Website Framework (GWF), kwani utachangia wananchi kupata taarifa, elimu na maelekezo kupitia tovuti kwa wakati sahihi,” amesema Mkumbo.

Naye Afisa TEHAMA wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Beatrice Ngutu, amesema mafunzo hayo yamemjengea uwezo wa ku-

shirikiana na Afisa Habari wake kuhakikisha tovuti yao inakuwa hai kila wakati, na wananchi wanapata taarifa zote muhimu ambazo awali walikuwa wanatumia muda mrefu kuzipata.

Ameongeza kuwa mafunzo haya yata-rahisisha upatikanaji wa taarifa na huduma mbalimbali kulingana na taarifa zilizo-ko katika tovuti zao.

Kwa upande wake, Afisa Habari wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Bi. Yasinta

lakini kutokana na kukosa ujuzi sahihi waliamua kumkabidhi mtu kwa ajili ya kuiendesha na hivyo kutokuwa na umiliki kamili wa namna ya kutoa taarifa kulingana na mahitaji ya wananchi wa Halmashauri yetu; lakini sasa itakuwa bora zaidi,” ameingiza.

Amesema kuwepo kwa tovuti kutasaidia kuondoa urasimu katika ofisi za Serikali, hususani matangazo ya zabuni, ambapo sasa yatapatikana kwenye tovuti badala ya kuwasiliana na afisa ili kupeana kwa upendeleo.



**Mmoja wa wakufunzi wa uundwaji wa tovuti (kushoto) akitoa maelekezo kwa Afisa Habari wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe, Tusa Mwambenja, katika mafunzo yaliyofanyika mjini Dodoma mwezi Machi, 2017. (Picha kwa hisani ya Mroki Mroki wa Habari Leo)**

Kisime, amesema mafunzo hayo yatasaidia kuifanya tovuti ya Halmashauri yake kuwa na muonekano tofauti na awali, ambapo tovuti zilizokuwepo hazikuwa na taarifa za wakati na mara nyingine kutokupatikana mtandaoni.

“Awali Halmashauri ilikuwa na tovuti,

Kwa upande wake, Afisa Habari wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, John Kilua, amesema mafunzo hayo yameletwa kwa wakati kwani hivi sasa kizazi kilichopo kinategemea kupata taarifa mitandaoni, na hivyo itarahisisha sana upatikanaji wa haraka wa taarifa kwa wakati wowote kwa kutumia simu za mkononi zilizounganishwa na intaneti.

“Tovuti hii tuliyoandaa itasaidia kutoa taarifa na maelekezo mbalimbali kwa wananchi kama vile mikutano ya

Baraza la Madiwani na miongozo ya namna ya kupata leseni za biashara na miongozo mingine ya kupata huduma mbalimbali,” amesema.

**Chanzo: Mbeya Yetu Blog**

**KUTOKA KIGOMA:****DC Kigoma aagiza Maafisa Habari wapewe ushirikiano**

**W**atendaji wa Serikali katika Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri nchini, wameagizwa kuwapa ushirikiano Maafisa Habari na TEHAMA, ili kuwawezesha kutoa taarifa za maendeleo kwa wakati kupitia tovuti za Serikali.

Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Samson Anga, ameyasema hayo wakati akifunga mafunzo ya kuandaa tovuti, sanjari na kuzindua tovuti hizo kwa Halmashauri 21 za mikoa ya Katavi, Kigoma na Tabora.

Amesema kuwa zama za urasimu zimepitwa na wakati, hivyo maafisa wa Serikali hawana budi kubadilika ili kuwawezesha wananchi kupata habari mbalimbali za serikali kwa wakati.

“Hili tutalisimamia na kuhakikisha kwamba suala la uwazi kati ya Serikali na wananchi wake linapewa kipaumbele. Karne za urasimu na kubania taarifa zilishapitwa na wakati, na sisi kama nchi tunasisitiza utawala bora kwa kushirikisha wananchi katika shughuli za maendeleo,” amefafanua Mkuu wa Wilaya.

Ameongeza: “Binafsi kama Mkuu wa Wilaya, nitahakikisha hili halitokei, na endapo litatokea basi huyo aliyesababisha ajandae.”

Amesema tovuti hizo ni njia mujarabu kwa Serikali kuwafikia wananchi na wananchi kutoa mrejesho kwa serikali yao kwa changamoto zinazowakabili na mambo ya msingi ya maendeleo.

Amewasisitiza pia maafisa hao kufanya kazi kwa weledi kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati kwenye maeneo yao, ili kuwawezesha wananchi kupata taarifa hizo na

pia kuwawezesha utawala bora na uwajibikaji Serikalini.

Amesema kuwa suala la utandawazi limetamalaki duniani kote, na kwamba ni lazima wafanye kazi na kwenda na mabadiliko hayo ili kuleta tija na ufanisi kwenye maeneo yao.

“Tusipokwenda sambamba na mabadiliko yanayotokea duniani, tukajifungia, tutaachwa na tusiwe na wa kumlaumu,” alionya Mheshimiwa Anga.

Amewashukuru wafadhili wa Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) kwa kushirikiana na Serikali kwa kutoa mafunzo hayo kwa maafisa hao na kufanikisha kufanya uzinduzi wa tovuti hizo. “Nawapongeza wenzetu PS3 chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kwa utayari wao bila ubaguzi na kufanya mafunzo haya kwa mikoa yote Tanzania, ukiacha ile 13 ambayo Mradi unatekelezwa,” amefafanua.

Kwa upande wake, Meneja wa Mradi wa PS3 Mkoa wa Kigoma, Simon Mabagala, amesema mafunzo hayo ya tovuti ya wiki moja yalihudhuriwa na jumla ya washiriki 42 kutoka Halmashauri za mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi, yakiwa na lengo la kuwawezesha Maafisa Habari kupata taarifa mba-

*“Tusipokwenda sambamba na mabadiliko yanayotokea duniani, tukajifungia, tutaachwa na tusiwe na wa kumlaumu - Samson Anga,*

**Mkuu wa Wilaya ya Kigoma**

limbali muhimu kwa ajili ya kuzifikisha kwa wananchi.

Naye Mwezeshaji Kiongozi wa Mafunzo hayo, Jackton Bikombo, amesema mafunzo ya utengenezaji tovuti yamekuwa ni ya mafanikio makubwa, na kwamba kuzinduliwa kwa tovuti hizo kutawawezesha wananchi kupata taarifa na kuondokana na changamoto ambazo zinasababisha wao kwenda kuulizia taarifa hizo kwenye Halmashauri zao.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki, Afisa Habari kutoka Halmashauri ya Kakonko, Cosmas Makalla, amewashukuru wafadhili, Mradi wa PS3 na Serikali kwa kuwapatia mafunzo hayo, kiasi cha kuwawezesha wao wenyewe kuandaa tovuti za Halmashauri zao.

“Sasa tumeiva, tunaahidi tutatekeleza majukumu yetu ili kuhakikisha taarifa hizi zinawafikia wananchi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu,” amesema.

Uzinduzi wa tovuti hizo utaboresha usimamizi wa ndani na ufanisi kwa kuongeza urahisi wa upatikanaji wa taarifa na nyaraka muhimu kwa wananchi, kuanzisha hifadhi ya taarifa za Halmashauri, kuboresha mawasiliano ndani ya Tamisemi na Serikali Kuu.

Vilevile, uzinduzi wa tovuti hizo ni sehemu ya uzinduzi wa tovuti kwa Sekretarieti za Mikoa yote 26 ya Tanzania bara na Halmashauri 185 zilizoinduliwa mjini Dodoma na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), George Simbachawene.

**Chanzo: Habari Leo**



## KUTOKA MWANZA:

## Maafisa TEHAMA na Mawasiliano watakiwa kutumia njia za kisasa za mawasiliano

**M**aafisa TEHAMA na Mawasiliano kutoka Mikoa mitano na Halmashauri 30 za Kanda ya Ziwa inayojumuisha Mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara, Shinyanga na Simiyu, wametakiwa kutumia njia za haraka na za kisasa katika mawasiliano, ikiwemo matumizi ya tovuti na mitandao ya kijamii ili kutangaza shughuli na mafanikio ya Serikali kwa umma.

Hayo yamesemwa jijini Mwanza na Mkurugenzi wa Habari na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Hassan Abbas, wakati wa uzinduzi wa tovuti za Mikoa na Halmashauri za Kanda ya Ziwa.

Aidha, Dkt. Abbas amesema uzinduzi wa tovuti katika Mikoa na Halmashauri hizo ni kigezo muhimu kitakachotumiwa na

Serikali katika kupima utendaji kazi wa Maafisa Habari katika kushughulikia kero na changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Dkt. Abbas ameingiza kuwa lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba tovuti za Mikoa na Halmashauri nchini zinaendelea kuwa hai na zenye taarifa zilizozingatia weledi na kwa wakati, na hilo litawezekana iwapo Maafisa Habari watatimiza malengo wanayopaswa kujiwekea katika maeneo yao ya kazi.

“Litakuwa si jambo jema kama baada ya muda mfupi tovuti hizi zitakufa kwa kubaki bila kuhuishwa. Kwa hiyo, kila mmoja kwa nafasi yake hana budi kuhakikisha kuwa tovuti hizi zinahuishwa mara kwa mara ili enzi mchango

endelevu wa Serikali na wafadhili,” amesema Dkt. Abbas.

Dkt. Abbas ameingiza kuwa pamoja na kuwepo kwa vyombo mbalimbali vya habari vinavyotumika kufikisha taarifa kwa wananchi ikiwa ni pamoja na magazeti na redio, bado tovuti na mitandao ya jamii vimeendelea kutumiwa na wananchi wengi.

“Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, hivi sasa Watanzania zaidi ya milioni 19 wapo mtandaoni,” amesema Dkt. Abbas.

Naye Mkurugenzi wa Miundombinu wa Wakala ya Serikali Mtandao (eGA), Bw. Benjamin Dotto, amesema Maafisa Habari na TEHAMA wanatakiwa kuwa wabunifu, wawumbuzi, na siku zote kujibidisha katika kuongeza viwango vya utendaji.

“Ni matumaini yangu kuwa baada ya kutumia framework hiyo mtatoa maoni ili kuiboresha Zaidi. Vilevile, wataalamu wetu wametoa technical na user manual za jinsi ya kutumia Framework hiyo, hivyo manual hizo zitumike ili pale inapoletwa taarifa ya kushindwa kufanya jambo, inakuwa na mantiki zaidi,” ameeleza Bw. Dotto.

Mafunzo hayo yaliyoanza tarehe 13 hadi 20 Februari 2017, yalifadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kupitia Mradi wa Uimarishaji Mifumo ya Sekta za Umma (PS3) na kusimamiwa na Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wakala ya Serikali Mtandao (eGA).

**Chanzo: Tovuti ya eGA**



**Mkurugenzi wa Idara ya Habari (Maelezo), Dkt. Hassan Abbas (katikati) akizungumza na washiriki wa mafunzo ya uandaaji wa tovuti. Kushoto ni Mkurugenzi Msaidizi wa Miundombinu ya TEHAMA kutoka OR-Tamisemi, Baltazar Kibola, na kulia ni Mshauri wa Habari na Mawasiliano kutoka PS3, Leah Mwainyekule (Picha kwa hisani ya Mroki Mroki, wa Habari Leo)**

## Simbachawene: Hatutamvumilia yeyote

Tarehe 27 Machi, 2017, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa George Simbachawene, alizindua tovuti mpya za Mikoa 26 ya Tanzania bara, na Halmashauri zake zote 185. Uzinduzi huo uliofanyika mjini Dodoma, ulihudhuriwa pia na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Harrison Mwakyembe, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, na Wakurugenzi wa Halmashauri. Hivi karibuni, **Mshauri wa Habari na Mawasiliano wa PS3, Leah Mwainyekule**, alifanya mahojiano maalum na Waziri Simbachawene kuhusu tovuti hizo mpya, hasa namna Serikali ilivyojipanga kuhakikisha kwamba tovuti hizo zinaendelezwa, kwa ajili ya manufaa ya mwananchi wa Tanzania...

**SWALI:** Tangu nchi yetu ipate uhuru mwaka 1961 haijawahi kutokea kwa taasisi zote za Serikali kuwa na tovuti zake. Hivi karibuni tumeshuhudia uzinduzi wa tovuti za mikoa 26 pamoja na Halmashauri 185, hili unalizingumziaje?

**JIBU:** Nakushukuru kwa swali lako zuri. Tangu nchi yetu ipate uhuru mwaka 1961 ni takribani miongo mitano, na kila muongo umekuwa na mafanikio na changamoto zake mbalimbali. Kadri dunia inavyoendelea na kuzidi kubadilika, teknolojia nayo imekuwa ikikua kwa kasi. Nakumbuka miaka ile ya zamani hatukuwa na huduma ya intaneti, lakini tumepiga hatua kutoka huko ambapo tulikuwa tunapashana habari kupitia njia nyingine za kizamani kama magazeti na redio, hadi kufikia sasa ambapo tunaweza kupashana habari kupitia tovuti na mitandao mbalimbali ya kijamii.

Kwahiyo leo hii tunavyozungumzia mafanikio yaliyotokana na utekelezaji wa Mradi wa Uimarishaji wa Mifumo ya Sekta za Umma (PS3), tunajivunia manufaa makubwa tuliyoapata ambayo yanatufanya tuingie kwenye zama za dunia ya kisasa, dunia inayoweka wazi na mambo yake kuwa wazi ili wananchi waweze kujua masuala yanayowahusu kwa ajili ya maendeleo yao. Ikumbukwe kuwa Tanzania iliweka saina Azimio la “Open Government Partnership” mwaka 2011, kuweka uwazi wa shughuli za Serikali kwa wananchi, ikiwa na lengo la kuimarisha utawala bora, kuongeza uwajibikaji wa Serikali, kuboresha utoaji wa huduma kwa umma, kuondoa rushwa, na Serikali kujenga imani

kwa wananchi wake. Kwenye eneo la uwazi, Azimio linaweka msisitizo kwa wananchi kupata taarifa kwa wakati, na uhuru zaidi. Na hili sio jambo geni wala jipya, sababu wananchi kupata taarifa zote za Serikali ni haki yao na haki hii imeelezwa pamoja na vifungu vingine vya kikatiba. Lakini kile Kifungu cha 8 kinachosema Mamlaka ya utawala wa nchi unatokana na wananchi, na hivyo wananchi wana haki ya kujua masuala yote yanayoendelea ambao wana maslahi nayo, hivyo wao ndio wenye maslahi ya moja kwa moja na maendeleo hayo.

Kwahiyo tunapoanzisha tovuti za Mikoa na Halmashauri kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, ikumbukwe kuwa tunakwenda kuwagusa wananchi wa kawaida waliopo katika maeneo hayo. Hakika, haya ni maendeleo makubwa na ni njia bora na nyepesi ya kuwafanya wananchi hawa wa kileo ambao wengi wao wana uwezo wa kupata mawasiliano ya mtandao wa intaneti kupitia simu zao za mikononi, kufahamu mambo mengi yanayohusu mamlaka zao za serikali za mitaa.



**Waziri wa Nchi, OR-TAMISEMI, Mhe. George Simbachawene, akitoa hotuba wakati wa uzinduzi wa tovuti za Mikoa na Halmashauri mjini Dodoma, Machi 27, 2017. (Picha kwa hisani ya Mroki Mroki wa Habari Leo)**

## UM NA WAZIRI WA TAMISEMI:

## e atakayetaka kukwamisha tovuti za Serikali

Hii ikiwa ni pamoja na fursa, upashanaji habari lakini pia changamoto zilizopo, na hata kuuliza maswali na kujibiwa kupitia tovuti hizo za Mamlaka ya Serikali za Mitaa zote 185 za nchi nzima.

**SWALI:** Watu wanaofuatilia masuala ya utawala bora wamekuwa wakitoa changamoto hususani kwa nchi za Afrika kufuata utawala wa sheria. Je, hizi tovuti ambazo zimetoka kuzinduliwa zitalizingatiaje hilo kwa maana ya kusisitiza katika masuala ya utawala bora, utawala wa sheria na hasa kwa kufuata matakwa ya wananchi?

**JIBU:** Ni kweli kwamba misingi ya utawala bora na utawala wa sheria ni kuwa na Serikali ya uwazi, ambayo wananchi wake wanaelewa namna inavyoendeshwa na kufanya mambo yake. Inawezekana kuwa nchi nyingi za Afrika zinalalamikiwa juu ya jambo hili, lakini kwetu sisi, leo tunavyozungumza, Halmashauri zote zimeunganishwa na zina tovuti zake. Kwa mfano, leo hii unaweza tu ukaandika [www.mpwapwadc.go.tz](http://www.mpwapwadc.go.tz) ukifungua pale unapata Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, au ukitaka kufungua tovuti ya Mpanda, [www.mpandadc.go.tz](http://www.mpandadc.go.tz) utajionea mambo yanavyoyokwenda kule na kujionea fursa zilizo ko Mpanda, mipango ya Halmashauri ya Mpanda, miradi inayotekelezwa, lakini pia unaweza ukauliza na ukajibiwa. Hii ni hatua kubwa na ambayo sasa inaifanya Tanzania isiwe miongoni mwa nchi ambazo si za kidemokrasia. Kwahiyo suala la uwazi la



**Mshauri wa Habari na Mawasiliano wa PS3, Leah Mwainyekule (kulia), akifanya mahojiano maalum na Waziri wa Nchi, OR-TAMISEMI, Mhe. George Simbachawene, katika yake mjini Dodoma hivi karibuni. (Picha na OR-TAMISEMI)**

Serikali kwa wananchi wake ni msingi muhimu sana wa falsafa zinazozungumzia suala la demokrasia na haki ya wananchi.

**SWALI:** Naona Mheshimiwa umeifagilia halmashauri yako ya Mpwapwa ambako umetokea; sasa kumekuwa na madai kutoka wananchi wakisema kwamba tovuti za Serikali mara nyingi hazina habari mpya kwa maana kwamba zinakuwa zimekaa tu, hakuna habari ambayo huwa inapandishwa kila siku. Kuna mikakati yoyote ambayo mmeiandaa ili kuhakikisha tovuti hizi za Mikoa na Halmashauri zilizoinduliwa zinakuwa sio gofu la habari, lakini zinaendelea kuzalisha habari siku baada ya siku ili wananchi waweze kujua yale yanayotokea kwenye maeneo yao?

**JIBU:** Kwanza, mkakati wa kwanza ulikuwa ni kukubaliana kuingia kwenye mradi wa PS3; kwamba tuingie huku kwa sababu tulitaka uwazi na kupeleka habari za wakati huo huo. Huko nyuma mfumo uliokuwa unatumika kwenye mamlaka

zetu za Serikali za Mitaa ilikuwa ni kuandika kwenye mbao za matangazo ambapo unaweza kuta haubadiliki hata kwa miezi mitatu, miezi sita. Sasa haikuwa tena ni jokofu la habari bali kilikuwa ni kitu cha tofauti kabisa ambacho ni kama vile gofu, kwamba zile habari zimepitwa kabisa maana habari lazima iwe ya wakati huo huo. Habari ikiwa ya muda mrefu inageuka kuwa historia, na mambo yanaenda kwa spidi sana, kwahiyo moja ya hatua ya muhimu ilikuwa ni hiyo ya kuhakikisha kwamba tunaingia kwenye mradi huu na tumefurahi kwamba mradhi umefanikiwa vizuri.

Na tulipokuwa tunazindua, nilisema kwamba lazima jukumu hili la kuhakikisha tunapata habari hizi liende sambamba na wajibu kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwahiyo, tumewaagiza viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa wanawawezesha Maafisa Habari wao ili waweze kutekeleza vizuri majukumu yao. Utakumbuka kuwa niliwaagiza Wakuu wa Mikoa wasimamie hili na wahakikisha kuwa Maafisa Habari na Maafisa TEHAMA wa Mikoa na Halmashauri wanakuwa na vifaa wezeshi kama kamera, kompyuta mpakato na intaneti, ili waweze kuzikusanya na kuzihariri na kuziweka habari hizi katika tovuti zao. Aidha, wahakikisha kuwa tovuti za Mikoa na Halmashauri zinakuwa na taarifa za kutosha na zinatolewa kwa wakati. Pia nimewaagiza Wakuu wa Mikoa wazisimamie mamlaka zao za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa Maafisa Habari wa Mikoa na Halmashauri wanashiriki katika shughuli zote za Mikoa na Halmashauri na kuingia katika vikao vyote muhimu.

**Inaendelea ukurasa wa 20**

**Inatoka ukurasa wa 19**

*“Wananchi wanapaswa kufahamishwa kuwa wakihitaji kupata habari za mamlaka zao za Serikali za Mitaa au Halmashauri, wanapaswa kuingia kwenye tovuti za Mikoa na Halmashauri zao husika” - Waziri wa Nchi, OR-TAMISEMI, Mh. George Simbachawene*



**Waziri wa Nchi, OR-TAMISEMI, Mhe. George Simbachawene, wakati wa mahojiano na mwandishi wa Makala haya, ofisini kwake mjini Dodoma. (Picha na OR-TAMISEMI)**

Huko nyuma Maafisa Habari walikuwa hawaingii kwenye vikao muhimu na hivyo kushindwa kupata taarifa za kuweka kwenye tovuti. Maafisa Habari wa Mikoa na Halmashauri wana fursa ya kushiriki vikao kama kile cha Kamati ya Fedha na Uongozi, au kikao cha Baraza la Madiwani na kwenye kamati mbalimbali. Ni lazima Maafisa Habari waingie huko ili waweze kuzitautau habari na kuzichuja na baadae kuzihariri ili ziweze kuwafikia wananchi.

Tumeagiza kwamba tovuti hizi zitumike kuboresha huduma kwa wananchi, kutangaza maeneo ya uwekezaji, kutekeleza masuala ya utawala bora na hasa uwazi na ushirikishwaji wa wananchi. Tumeagiza pia miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali katika Mikoa na Halmashauri itangazwe vyema pamoja na taarifa za bajeti ziwepo kwenye hizo tovuti.

Tumeagiza kwamba Maafisa Habari wahakikishe kuwa wananchi wanafahamu uwepo wa tovuti hizi, maana inaweza ikawa ipo lakini wananchi hawafahamu. Kwahiyo natarajia kuanza kusikia Halmashauri zikiwatangazia wananchi wao kuwepo kwa tovuti hizi kupitia vyombo vya habari mbalimbali yakiwemo magazeti, redio na televisheni.

Wananchi wanapaswa kufahamishwa kuwa wakihitaji kupata habari za mamlaka zao za Serikali za Mitaa au Halmashauri, wanapaswa kuingia kwenye tovuti za Mikoa na Halmashauri zao husika. Pia, tumesisitiza kwamba wahakikishe malalamiko ya wananchi yanajibiwa kwa wakati.

Lakini siyo malalamiko tu, wananchi wanaweza kuwa na maswali pia. Maswali yatakayoulizwa kwa njia ya tovuti yanapaswa kujibiwa kwa haraka. Lengo ni kuhakikisha kuwa tovuti za Mikoa na Halmashauri zinakuwa na habari zilizokamilika na kuhakikisha kuwa wananchi wanashiriki vizuri katika mipango, katika mikakati na katika maendeleo ya Halmashauri zao, maana mamlaka ya nchi yetu yanatoka kwa wananchi.

**SWALI:** Sasa Mheshimiwa Waziri, kuna namna yoyote ambayo mmepanga ili kuhakikisha kwamba maagizo uliyoyatoa yanatekelezwa; yaani ile *‘output’* (matokeo) inapimwaje? Kuna

vigezo vyovyote ambavyo mmeviweka kwa ajili ya kupima kwamba, ndio maagizo yametolewa, lakini haya maagizo yamefuatwa na yanatekelezwa?

**JIBU:** Tunayo maagizo mengi, na kama unavyofahamu, Wizara hii ni Wizara ya Utawala hasa, kazi yake ni kuhakikisha kuwa viungo vyote vya mwili vinafanya kazi. Serikali za Mitaa ni kama mwili wa binadamu, na TAMISEMI ni kama kichwa; lazima kihakikishe mikono, miguu, viungo vyote vya mwili vinafanya kazi. Kwahiyo kama tulivyowapa *‘target’* za mambo mengine, pia katika jambo hili litakuwa ni eneo la kuwapima. Uzuri wa jambo hili halina shida sana namna ya kupima, mimi nitaingia katika intaneti yangu hapa nikiingia kwenye kompyuta yangu nikibonyeza, nikitaka kuangalia basi nikikuta hawamo au hawajaweka taarifa za leo leo basi hatua naichukua kuanzia wakati ule. Kwahiyo ni jambo rahisi namna ya *‘kucontrol’* na kudhibiti, lakini pia tutajaribu kuweka utaratibu wa namna ya kuwapima ambao utakuwa wa wazi lakini pia tutawapima kwa vigezo na hata kuwa tunatangaza hata mshindi wa kwanza, wa pili, mpaka wa mwisho.

**UM NA WAZIRI WA TAMISEMI:**

**SWALI:** Wakati mnafikiria kuwapima, iko changamoto moja kubwa sana ambazo hizi ofisi za Serikali inazo, ambayo na hii linalohusiana na Maafisa Habari, hususani katika Halmashauri. Kuna Halmashauri nyingi sana ambazo hazina kabisa Maafisa Habari, wakati ziko nyingine chache ambazo zinaweza zikawa na Maafisa Habari wawili au watatu, au pengine mmoja. Sasa wakati mnafikiria kuwapima utendaji wao katika kupandisha habari katika tovuti, hili suala la changamoto la kutokuwepo kwa Maafisa Habari mnalishughulikia vipi?

**JIBU:** Changamoto za upungufu wa watumishi uko kila mahali lakini habari nini? Habari ni taarifa zinazohusu matukio yanayohaririwa vyema kwa ajili ya kurushwa na vyombo vya habari. Mamlaka za Serikali za Mitaa zina wajibu kuwapa wananchi taarifa mbalimbali za mambo yanayowahusu wananchi wao. Wakati mwingine jukumu hilo litokane na taaluma ya kawaida kabisa ya ufahamu wa mambo haya ya kimtandao. Kwahiyo la kwanza, isitokee Halmashauri yoyote ikawa na kisingizio cha kutokufanya haya niliyowaagiza eti kwasababu hawana Maafisa Habari. Hatutumvumilia atakayetaka

kukwamisha hili. La pili Halmashauri zote zihakikishe zinatoa habari kwa wananchi, hata kama hazina Afisa Habari, kwasababu habari zinajulikana. Tatu, tujitahidi kuweka mfumo ambao utatusaidia ili tuweke katika vipaumbele vya ajira tutakazozipata sasa ili kuajiri Maafisa Habari.

Lakini kama mnavyofahamu, kuna upungufu wa kada mbalimbali wakiwepo manesi, walimu... kwahiyo na hili la Maafisa Habari kutokana na umuhimu wake tutalipa kipaumbele, lakini isiwe sababu ya mamlaka yoyote ya Serikali za Mitaa kuona kwamba haiwezi kuweka habari kwasababu haina Afisa Habari.

**SWALI:** Sasa maadam umetoa agizo hilo, hudhani kama kuna umuhimu sasa wa kuwawezesha wale ambao watakuwa wanaendelea kusaidia katika kuzitafuta na kuziweka habari katika tovuti wakati mnasubiri ofisi hizi nyingine za Serikali zisizo na Maafisa Habari waweze kuajiri Afisa Habari? Yaani mnawawezeshaje ili waweze kufanya ile kazi iliyotakiwa kufanywa na Afisa Habari?

**JIBU:** Kama nilivyosema, Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni mamlaka zilizojitosheleza kwa maana wanaweza kuamua na kupanga wana Rasilimali Watu, na Rasilimali Fedha. Wakiamua kupanga kama kipaumbele kwao, wanaweza hata kutafuta mtu wa kuwafundisha kwa muda wa kuwasaidia, lakini wanaweza kuteua mtu mmoja miongoni mwao, ambao kama nilivyosema, hakuna utaalum mkubwa sana katika kuizingiza hizi taarifa kwenye tovuti zao. Kwahiyo nisihi tu kwamba wachukue agizo langu na watekeleze hivyo, lakini pia wafanye mikakati kuhakikisha wanawapata watu wanaoweza kufanya hizo kazi vizuri. Lakini na sisi Serikali tutaona namna ya kufanya kutokana na ikama mbalimbali, tuone kwenye hiyo kada tunafanya nini.

**SWALI:** Mheshimiwa Waziri, PS3 inafanya kazi katika Mikoa 13 na Halmashauri 93 za Tanzania bara, lakini katika hili suala la tovuti tulialika mikoa yote 26 pamoja na maafisa kutoka Halmashauri zote 185. Bahati mbaya sana kuna baadhi ya maeneo ambayo mradi haufanyi kazi, ambapo walishindwa kuwatumaa maafisa wao kwa ajili ya kuja kwenye mafunzo ya kupata tovuti. Sasa kuna hili suala la 'hosting' ambalo liko kule upande wa eGA; kama walishindwa kutuma maafisa wao kuja kwa ajili ya kuhudhuria mafunzo na kuanzisha tovuti zao, wataweza kweli kuendelea hizi tovuti ambazo zimeandaliwa kwa maana ya kulipia 'hosting' kule eGA?

**JIBU:** Kama mlezi wa Halmashauri zote nchini, matamano yangu ni kuona PS3 inapanuka. Ni imani yangu kwamba sababu hili tumekamilisha na limefanikiwa, basi tunaanza kwenye hiyo awamu nyingine. Sasa kama hawa tuna-waacha njiani, tutakuwa hatujawatendea haki. Kwahiyo niseme tu wao wajitahidi kwa wajibu walionao kuweza kutimiza wajibu wao ili waweze kuingia kwenye mifumo hii ya uwazi na urahisi wa kuleta maendeleo kwenye mamlaka zao, lakini niwaombe PS3 na nyie mjitahidi basi kwenda kwenye awamu nyingine.



**Baadhi ya wafanyakazi wa PS3 na eGA wakifuatilia matukio mbalimbali wakati wa hafla ya uzinduzi wa tovuti za Mikoa na Halmashauri mjini Dodoma, Machi 27, 2017. (Picha kwa hisani ya Mroki Mroki wa Habari Leo)**

## Matukio Mbalimbali wakati wa Uzinduzi wa

*Picha zote kwa hisani ya M*



**Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Harrison Mwakyembe, akizungumza wakati wa uzinduzi wa tovuti mjini Dodoma.**



**Msanii Mrisho Mpoto akighani kwa hisia wakati wa hafla ya uzinduzi wa tovuti mjini Dodoma.**



**Wafanyakazi wa PS3 wakiwa katika picha ya pamoja na meza kuu, wakati wa hafla ya uzinduzi wa tovuti iliyofanyika mjini Dodoma.**



**Baadhi ya Wakuu wa mikoa wakishangilia uzinduzi wa tovuti mjini Dodoma. Kutoka kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mhe. Luteni Chiku Galawa, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Mhe. Joel Bendera, na Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mhe. Godfrey Zambi.**

## **Kitaifa wa Tovuti za Mikoa na Halmashauri**

*Mroki Mroki wa Habari Leo*



**Mkurugenzi wa Mradi wa PS3, Dkt. Emmanuel Malangalila, akielezea kazi za PS3 wakati wa uzinduzi wa tovuti mjini Dodoma.**




**Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Rehema Madenge, akitoa neno la shukrani wakati wa hafla ya uzinduzi wa tovuti za Mikoa na Halmashauri, iliyofanyika mjini Dodoma.**



**Kiongozi wa Timu ya Mifumo ya Mawasiliano ya PS3, Desderi Wengaa, akifuatilia matukio wakati wa hafla ya uzinduzi wa tovuti mjini Dodoma.**



**Msanii Mrisho Mpoto akitumbuiza wakati wa hafla ya uzinduzi wa tovuti za Mikoa na Halmashauri, iliyofanyika mjini Dodoma.**



# MIFUMO YETU

